BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 01 Machi, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

146. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na changamoto katika kutoza kodi ya miundombinu kwa watalii wanaolala katika hoteli za Zanzibar licha ya mifumo iliyopo ya ulipaji kodi kupitia Mamlaka za Kukusanya Kodi Zanzibar. Changamoto hii imeleta malalamiko makubwa kwa watalii wanaoingia na kutoka Zanzibar.

(a) Je, ni nani haswa anayepaswa kumtoza mgeni kodi ya miundombinu, na ni taratibu gani Serikali inazozisimamia ili kutatua suala hili.

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani madhubuti za kurekebisha mfumo wa utozaji kodi ya miundombinu ili kupunguza malalamiko ya watalii wanaolala katika hoteli za Zanzibar.

(c) Je, ni mikakati gani inayochukuliwa na Serikali kuhusu utozaji wa kodi ya miundombinu kwa watalii ili kuboresha uwazi na kuhakikisha kuwa kodi hizo zinatozwa kwa njia inayofaa kwa kuzingatia sheria za nchi.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

62. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na utaratibu usio rasmi, unaogharimu na usiowafurahisha wananchi walio wengi wa kuendesha kambi za kusomea maskulini hasa kwa madarasa yaliyokabiliwa na mitihani ya Taifa, huku Serikali nayo haijalitolea kauli rasmi jambo hili pamoja na kulifahamu kwake.

(a) Je, ni jambo gani linalolazimisha maskuli kuweka kambi katika mazingira ambayo sio rasmi na rafiki kwa watoto.

(b) Je, Serikali haioni ulazima wa kuwa na mtaala unaoruhusu kusomeshwa na kudurusiwa ndani ya muda uliopangwa kwa madarasa yenye mitihani ya Taifa ili kuepusha ulazima wa kuweka kambi maskulini.

(c) Kama Serikali imehakikisha kwamba kambi ni njia bora ya kuongeza ufaulu na ufanisi wa wanafunzi na skuli, je, kwa nini haitengenezi utaratibu wa kuzirasimisha kambi katika maskuli kwa madarasa yenye mitihani ya Taifa.

80. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Changamoto ya uvujaji wa skuli ya Kitogani inawalazimisha wanafunzi wa skuli hiyo, kuakhirisha masomo wakati wa mvua zinaponyesha.

(a) Je, Wizara yako imewahi kuifahamu changamoto hiyo.

(b) Je, ni lini skuli hiyo itafanyiwa ukarabati.

(c) Je, Serikali inawaelekeza nini wananchi wa shehia ya Kitogani.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

60. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Vyombo vya Habari vya Umma vikiwemo Gazeti la Zanzibar Leo, ZBC Radio na ZBC TV vinastahili pongezi kwa kuuhabarisha umma. Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kwamba asilimia kubwa ya habari na taarifa zinazotolewa na vyombo hivyo vinaonyesha zaidi taarifa na matukio ya viongozi wa chama tawala na sio kwa viongozi wa vyama vingine.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kutoa taarifa za viongozi wa chama tawala peke yake ni kuwanyima wananchi haki yao ya kupata taarifa na kuvinyima vyombo vyetu uhuru wa kujiendesha kibiashara.

(b) Je, ni mambo gani yanavitafautisha vyombo vya Habari vya Serikali na vile vya vyama vya siasa.

(c) Je, kwa miaka mitatu iliyopita (2020/2021 – 2022/2023), ni matukio mangapi mubashara yamerushwa na ZBC Radio na ZBC TV yakihusisha chama tawala na yakihusisha vyama vyengine.

131. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kuanzishwa kwa maktaba ya vitabu vya lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa ajenda muhimu ya Serikali yetu.

Je, tathmini iko vipi juu ya utekelezaji wa wazo hili.

Wizara ya Afya:

134. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, tathmini iko vipi juu ya ushiriki wa wanaume katika huduma za afya ya uzazi pamoja na huduma za uzazi wa mpango.

148. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Visiwa vya Kokota, Funzi na Mtambwe Mkuu ni visiwa vinavopatikana katika jimbo la Mtambwe ambavyo kwa kiasi kikubwa vilikuwa vikiitegemea hosptiali ya Wete kwa huduma za afya ikiwemo huduma ya mama na mtoto. Hata hivyo, kuhamishwa kwa hospitali ya Wete kwenda Kinyasini kumeleta usumbufu mkubwa kwa wakaazi wa visiwa hivi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya afya katika visiwa hivi ili kupunguza usumbufu kwa wananchi wanaohitaji huduma za afya na wanaolazimika kusafiri kwa masaa mengi kufuata matibabu Kinyasini.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka gari ya dharura katika hospitali ya Wete ili kuwasaidia wagonjwa walio katika hali mbaya kuwafikisha haraka katika Hospitali ya Kinyasini hususani wanaotokea katika visiwa.

<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>

83. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kujipatia ajira, wananchi wengi wa jimbo la Paje wanajiendeleza na kilimo cha ndimu, kama zao kuu la biashara.

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwatafutia soko la nje ya nchi wakulima hao.

(b) Je, ni lini utawatembelea wakulima hao pamoja na kujionea wanavyolima zao hilo.

(c) Je, unawaambia nini wakulima wa jimbo la Paje kuhusu biashara ya zao la ndimu.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

33. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali imeamua kuwawezesha vijana kujiajiri kwa kuruhusu biashara ya bodaboda kwa lengo la kujiajiri wenyewe. Pamoja na jambo hilo jema, kuna changamoto mbali mbali zinajitokeza.

(a) Je, hadi sasa kuna ajali ngapi zimejitokeza zilizosababishwa na usafiri wa bodaboda.

(b) Je, vifo na majeruhi wangapi waliosababishwa na usafiri wa bodaboda kwa mwaka 2023.

167. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

(a) Ni maeneo gani ambayo kwa sasa yananufaika na mawasiliano ya 5G hapa Zanzibar.

(b) Ni yepi matarajio ya Serikali katika kuziunganisha taasisi zake kwenye mfumo mmoja wa mawasiliano ili kurahisisha utendaji wa shughuli mbali mbali za Serikali kwa kasi na uweledi zaidi.

IV. HOJA ZA SERIKALI

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Zanzibar,
01 Machi, 2024.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.